



## MAKOSA YA KISEMANTIKI KATIKA MAWASILIANO ANDISHI YA KISWAHILI YA WANAFUNZI WA SHULE ZA UPILI NCHINI KENYA

ARUBA Beatrice Kemunto<sup>1</sup>, Prof. MOHOCHI Sangai Ernest<sup>2</sup>, Dkt. ONTIERI James Omari<sup>3</sup>

<sup>1</sup>Mwanafunzi, Chuo Kikuu Cha Maasai Mara - KENYA

<sup>2</sup>Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Rongo

<sup>3</sup>Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Maasai Mara

**Barua pepe:** beatricekemunto72@gmail.com, Smohochi@gmail.com, jontieri@gmail.com

**Ikisiri:** Lugha ni kipengele muhimu ambacho huwezesha kuwepo kwa mawasiliano miongoni mwa watu. Katika juhudi za kurahisisha uwasilishaji na upokeaji wa ujumbe, ni muhimu kuhakikisha kuwa lugha sahihi imetumiwa. Katika karne hii ya 21 ya mawasiliano ya sayansi na teknolojia, suala la mawasiliano limeshika kasi kubwa kwa kila mtu. Kwa namna hii mawasiliano yamekuwa ni jambo muhimu sana ambalo humwezesha mtu kupashana habari, taifa kutoa taarifa mbalimbali kwa wananchi kuhusu matukio, na hata malengo na mikakati iliyojiwekea. Iwapo makosa yatatokea katika maandishi au mazungumzo, mawasiliano kama shughuli kuu ya kibinadamu hayatafaulu. Madhumuni ya makala haya ni kuchanganua makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika mawasiliano andishi ya Kiswahili ya wanafunzi wa shule za upili. Makala haya yametumia nadharia ya Uchanganuzi Makosa (Corder, 1967) kuonyesha kuwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili hufanya makosa ambayo yanaweza kubainishwa, kuchanganuliwa, kuainishwa na kutathminiwa ili kubainisha mfumo unaofanya kazi. Data ya makala haya ilikusanywa kutoka kwa wanafunzi wa shule za upili hususani kidato cha tatu, kaunti ya Kakamega, nchini Kenya. Mbinu iliyotumiwa katika ukusanyaji wa data ni ya nyanjani (hojaji na mjarabu). Katika kubainisha makosa husika, makala haya yametumia vielelezo mbalimbali kutoka kwa watafitiwa lengwa. Makala haya pia yanatoa mapendekezo ya utatuzi wa makosa yanayojitokeza katika matini za wanafunzi wa shule za upili. Makala haya yatawafaidi walimu wa Kiswahili, wanafunzi wa shule za upili na vyuo vya elimu ya juu katika kurekebisha makosa ya kisemantiki katika matini anuwai.

**Maneno Muhimu:** Lugha, Semantiki, Makosa, Msimbo, Msamiati

### 1.0 Utangulizi

Kiswahili ni lugha ambayo huzungumzwa na takribani watu million mia moja kote ulimwenguni. Pia, ni lugha ya saba ulimwenguni na ya pili barani Afrika kwa kuwa ina wazungumzaji wengi (Bakari 1982,). Lugha ya Kiswahili imeenea kwingi katika Afrika Mashariki na sehemu zingine ulimwenguni. Mambo yaliyosaidia kuenea kwa lugha ya Kiswahili ni biashara ya watumwa, dini, ukoloni na harakati za kutafuta uhuru. Hadi sasa Kiswahili kinatangazwa katika stesheni nyingi za redio ulimwenguni, kwa mfano, *British Broadcasting Corporation* (BBC), *Voice of America* (VOA), Redio China, Sauti ya Ujerumani na kadhalika. Pia hufunzwa katika vyuo Vikuu vingi ulimwenguni, kwa mfano, Chuo Kikuu cha Bayreuth nchini Ujerumani, *School of*

*Oriental and Afrikan Studies* cha Chuo Kikuu cha Osaka nchini Japan na vingine vingi ulimwenguni.

Nchini Kenya Kiswahili sanifu ni lugha inayozungumzwa na watu idadi yake yakadiriwa kuwa zaidi ya milioni sitini (Mgullu, 1999). Hata hivyo, matokeo ya wanafunzi katika mitihani yao ya K.C.P.E na K.C.S.E hayaridishi katika somo la Kiswahili na yanaendelea kudorora. Washikadau wanadai kuwa makosa mbalimbali huchangia kuwepo kwa hali hii, yakiwemo makosa ya kisemantiki.

Makosa ya kisemantiki hutokea kutokana na uvunjaji wa sheria za mfumo wa kisemantiki katika lugha lengwa (kutojua sheria za lugha au kutambua sheria za lugha lengwa ambazo si sahihi) au utaratibu wa lugha fulani, na kusababisha ujumbe kutoeleweka na waliodhamiriwa (Obediat, 1986). Hivyo basi, kosa ni mchanganyiko wa maneno katika sentensi ambapo maana haijitokezi vizuri. TUKI (2004), kosa ni kufanya lisilo sahihi au lisilokubalika.

James (1995), aliyaaainisha makosa ya kisemantiki katika makundi matatu: ya kileksia, kisarufi na uwekaji maneno pamoja visivyo. Kosa la kileksia hutokea pale ambapo neno au msamiati fulani hutumiwa visivyo katika sentensi. Anaendelea kusema kuwa kutozingatia sarufi katika utungaji wa sentensi (sauti, maendelezi, uakifishaji, aina za maneno na kadhalika) huchangia makosa ya kisemantiki. Hivyo basi, katika maisha ya kila siku binadamu wanahitaji kuwasiliana ili kutimiza mahitaji ya msingi na yale ya ziada.

Anavyosema Wyrick (1979), ni muhimu kwa mwenye ujumbe fulani kuuhamisha katika maandishi kwa kutumia maneno mwafaka ili maana iwafikie wasomaji. Makosa yanapojitokeza katika maandishi hapatakuwa na mawasiliano na kwa hivyo lugha haitakuwa imetekeleza wajibu wake.

### **1.1 Dhana ya semantiki**

Wataalamu mbalimbali wameishughulikia taaluma hii kwa kina (Jackendoff, 1987; Lakoff, 1988; Katz, 1986; Newmey, 1993; Fauconnier, 1997; Tyler na Evans, 2003; Griffiths, 2006; Obuchi na Mukhwana, 2010 ). Wanapoitalii taaluma hii ya semantiki, hujishughulisha zaidi na uhusiano uliopo baina ya maana na muundo wa lugha, kwa kuwa maana ni kigezo muhimu katika kuelewa lugha. Katika taaluma hii, maana inayoshughulikiwa sana ni maana fikirika. Maana hii huyakusanya mambo ya kimsingi yanayofikirika. Kwa mfano, neno ‘msichana’ litakusanya uhusiano kama vile +uhai, +uuke, +uchanga na +binadamu. Kutokana na mfano huu, ni dhahiri kuwa maana fikirika ni maana inayokusanya mambo mbalimbali tunayoweza kuyafananisha au kuyahusisha na neno fulani.

Ijapokuwa masuala ya kimaana hutumika katika kubainisha maana za maneno, si rahisi kupata masuala ya kimaana yatakayoonyesha tofauti hizo katika baadhi ya maneno au kuonyesha tofauti hizo baina ya maneno kwa kuwa yanakaribiana sana kimaana. Hivyo basi, baadhi ya maneno huweza kutofautishwa au kuhusishwa na maneno mengine kwa kuurejelea uhusiano wa maneno hayo na maneno mengine. Pointer (2005) anasema kuwa katika semantiki ya maneno, neno moja linaweza kusheheni maana tofauti linapotumiwa katika muktadha. Kwa mfano, katika lugha ya Kiingereza kuna neno moja tu la kutajia hali zote za mchele ‘*rice*’. Katika lugha ya Kiswahili kuna takribani maneno sita ya kutajia mchele. Kwa mfano:

Mchele – mchele mbichi  
 Mpunga – mchele ukiwa shambani  
 Masendeya – mchele mbovu  
 Pilau – mchele uliopikwa kwa viungo  
 Biriani – mchele uliopikwa kwa birinzi  
 Wali – mchele uliopikwa

Ikiwa hakungekuwa na maneno hayo yote kueleza hali zote za mchele, basi neno moja ‘mchele’ lingetumiwa.

Obuchi na Mukhwana (2010) wanasema kuwa semantiki ni stadi ya maana na jukumu lake kuu ni kueleza maana ya maneno na dhana. Wanasemantiki hushughulikia maana katika viwango vya vipashio huru na maana ya vipashio hivyo katika tungo. Hii ina maana kuwa maana huchunguzwa katika viwango vya maneno katika sentensi. Jackendoff (1987), anaongezea kuwa semantiki huchunguza namna viambajengo vya lugha huhusiana ili kuleta maana kamilifu. Hivyo basi, semantiki kama taaluma ni muhimu kwani isipozingatiwa vyema, mawasiliano ya wanadamu hayawezi kusahilika kamwe. Hali hii inatokana na ukweli kuwa jukumu kuu la lugha ya mwanadamu ni mawasiliano ambayo huhusisha upashaji wa ujumbe.

### 1.1 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Shule kumi na mbili za upili katika kaunti ya Kakamega zilihusishwa katika kupata data ya makala haya. Uteuzi wa kuzingatia matabaka ya shule ulitumiwa kuteua shule husika. Wanafunzi kumi wa kidato cha tatu kutoka kila shule waliteuliwa ili kufanya mjarabu uliosaidia katika uchaganuzi wa makosa ya kisemantiki. Wanafunzi wa kidato cha tatu waliteuliwa katika kufanya mjarabu kwa kuwa wamefundishwa kwa kina matumizi ya lugha, utungaji wa sentensi na uandishi wa matini mbalimbali tangu kidato cha kwanza. Watafitiwa walipewa hojaji iliyokuwa huru na ambayo iliwahitaji kutoa habari za kibnafsi na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa jumla. Pia walipewa mjarabu uliowahitaji kutunga sentensi mbalimbali na kuandika insha juu ya **‘umuhimu wa magazeti kwa wanafunzi wa shule za upili’**. Baadaye insha 120 zilisahihishwa huku makosa ya kisemantiki yaliyojitokeza kubainishwa na kujadiliwa. Makosa yafuatayo ya kisemantiki yalibainishwa:

- i. Matumizi ya msamiati usiofaa
- ii. Kuunganisha maneno visivyoo
- iii. Kuacha sauti katika neno
- iv. Matumizi ya lugha ya kishairi
- v. Ufafanuzi uliokithiri
- vi. Mrundiko wa maneno katika sentensi
- vii. Matumizi ya msimbo wa sheng’
- viii. Kutumia sauti isiyofaa katika neno

Katika ari hiyo, makala haya yatahitimishwa kwa kuependekeza nafasi ya walimu, wanafunzi pamoja na Taasisi ya ukuzaji wa mitaala nchini Kenya, katika upunguzaji wa makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili.

### 1.2.1 Matumizi ya Msamiati Usiofaa

Makosa ya matumizi ya msamiati usiofaa hutokea pale ambapo mwanafunzi hupachika neno lisilofaa katika muktadha fulani. Msamiati alio nao unamkanganya na anautumia vibaya anapojaribu kujieleza katika lugha ya pili anayojifunza. Hali hii inapotokea, kunatokea athari ya kimaana kwa sababu neno linabadilisha maana iliyokusudiwa. Maneno ambayo ni visawe na vitate hubadilishwa na mwanafunzi hata bila mwanafunzi kugundua kama amefanya kosa. Hii ni kwa sababu maneno yanayokaribiana huweza kuwasilishwa pamoja katika ubongo wa binadamu na mwanafunzi huweza kuyatumia maneno hayo pasipo kutambua kuwa amesababisha makosa ya kimaana.

Mwanafunzi hubadilisha neno ili kuepukana na shida inayomkabili. Hali hii humfanya kutumia mbinu zake maalumu kuunda neno litakalofaa katika muktadha husika. Makosa haya yanayofanywa na mwanafunzi yanadhihirisha hali yake ya leksia katika ubongo wake. Kwa mfano, Taasisi ya elimu nchini Kenya (2000), iligundua kuwa wanafunzi wengi wa shule za msingi na za upili wanakumbwa na matatizo ya kimatamshi; uteuzi wa msamiati; sarufi na kuingiliana kwa lugha, hali ambayo huathiri mawasiliano. Baadhi ya wazungumzaji wanaeleweka kwa shida ilhali wengine hawaeleweki kabisa. Mifano ya makosa kutoka kwa watafitiwa:

- i. Baba alienda baharini *kumshika* papa <kuvua>.
- ii. Chungu kilichopikiwa samaki hunuka *chombo* <shombo>.
- iii. Magazeti *hujenga* msamiati wa Kiswahili <hukuza>.
- iv. Watasoma magazeti ili *wasikie* yanayoandikwa <waelewe>.

Katika mfano (i) hapo juu, mwanafunzi alitumia msamiati unaokaribiana sana kimaana lakini kisemantiki haufai katika kauli husika. Matumizi ya neno ‘**kushika**’ ambalo linarejelea dhana ya kushika mtu mkononi au kamata linapelekea kauli husika kuwa na kasoro. Hapa neno ‘**kuvua**’ lingefaa zaidi katika muktadha, likiwa na maana ya kunasa samaki kutoka majini. Katika (ii) inaonyesha matumizi mabaya ya vitate. Obuchi na mwenziwe (2010) wanasema:

“ Vitate ni maneno yanayokanganya kimatamshi kwa sababu sauti zao zinakaribiana. Ingawa sauti zinakaribiana, maneno hayo ni tofautu kimaana.”

Neno ‘**chombo**’ limetumika badala ya neno ‘**shombo**’ na kupelekea kauli husika kuwa na kasoro. Chombo lina maana ya kitu chochote cha kufanyia kazi na shombo ni harufu anayokuwa nayo samaki baada ya kuvuliwa. Katika mfano (iii), mwanafunzi alitumia neno ‘**jenga**’ likimaanisha kutengeneza nyumba na ‘**kuza**’ ni kitu kupata kuzidi. Maneno haya yalimkanganya mwanafunzi na kwa kutumia jenga badala ya kuza maana ilivurugika. Vilevile mfano uliopo katika (iv) neno ‘**wasikie**’ lilitumiwa visivyo badala ya neno ‘**kuelewa**.’ Neno *sikia* lina maana ya kupokea mawimbi ya sauti kwa kutumia sikio na neno *kuelewa* linalimaanisha kufahamu jambo ambalo ni mwafaka katika kauli husika liliachwa. Mwanafunzi aliathiriwa na lugha ya kwanza. Hii ni kwa sababu maneno haya ya lugha ya pili hayajaratibiwa vizuri katika leksigrafia ya mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili. Hali duni ya ujifunzaji wa lugha ya pili na ukosefu wa umilisi wa sheria za lugha ya pili katika hatua ya ujifunzaji huchangia kuwepo kwa makosa husika.

### 1.2.2 Kuunganisha Maneno Visivyo

Maneno yanapotumiwa katika sentensi hutarajiwa yawasilishe ujumbe muhimu. Yanapounganishwa na kuandikwa kama neno moja huwatatiza wasomaji. Maana inayokusudiwa inaweza kupotea na msomaji anaweza kupata maana isiyokusudiwa. Mipaka kati ya neno na neno inahitajika iwe wazi ili pasiwe na utata wakati wa kusoma maandishi. Maneno mawili au matatu yanapounganishwa huunda istilahi mpya za Kiswahili ambazo hutumiwa katika maandishi pasi kujua kama zinawasilisha maana au la. Katika nomino kuna baadhi yao ambazo huunganishwa na kuunda nomino moja inayokubalika na inayowasilisha dhana moja na wala si mbili. Kwa mfano, mbwa +mwitu = mbwamwitu (nomino+ nomino = nomino) lililo na maana ya mnyama wa jamii ya mbwa aishiye porini. Sentensi zifuatazo zinadhihirisha makosa ya kuunganishwa kwa maneno visivyo:

- i. Yohana anasifanjema <ana sifa njema>.
- ii. Mwalimu wa Kiswahili ana dukakubwa <duka kubwa>.

Maneno mawili hata matatu yaliunganishwa na kuunda istilahi moja ambayo haina maana. Katika (i) maneno matatu yaliunganishwa visivyo na kuunda neno moja ambalo hata kulitamka ni shida, 'anasifanjema' <ana sifa njema>. Kwa kufanya hivyo maana hupotea kwa sababu katika lugha ya Kiswahili na hata kamusi hamna neno lenye muundo wa aina hiyo. Maneno hayo ni tofauti na yalistahili kuwekewa nafasi ya kuyatenga ili ujumbe uweze kumfikia msomaji. Katika mfano (ii) neno 'duka' ambalo ni nomino limeunganishwa na neno 'kubwa' ambalo ni kivumishi na kupelekea kuwepo kwa kosa la kisemantiki. Haya makosa husababishwa na uzembe wa baadhi ya wanafunzi wa kutosoma kwa mapana ili kuwa na umilisi wa maneno yanayostahili kuunganishwa na katika kiwango kipi. Pia, kutomakinika hasa wanapoandika kazi zao na kuandika kwa haraka kwa baadhi ya wanafunzi huwafanya kutoacha nafasi inayostahili kati ya neno moja na lingine.

### 1.2.3 Kuacha Sauti katika Neno

Katika lugha yoyote ile neno huwa ni mkusanyiko wa sauti zinazowekwa pamoja na kuunda silabi ambayo kutamkwa kwa mpigo mmoja au kuandikwa na kuleta maana fulani. Obuchi na Mukhwana (2010), silabi ni kipashio cha kifonolojia kinachohusu matamshi na ambacho kwacho sauti za lugha hutamkwa mara moja kama fungu moja linalojitegemea. Fungu hilo linaweza kuwa lina sauti moja pekee, au linaweza kuwa na sauti mbili au zaidi kutegemea muundo wa lugha inayohusika. Neno lisiponakiliwa vizuri maana iliyotarajiwa haitamfikia msomaji na hapatakuwepo na mawasiliano. Makosa haya yalitokea kwa kuacha sauti moja au mbili.

- i. \*Mag eti yana umuhimu lakini wanafunzi hawa emi
- ii. \*Ni vi uxi kusoma magazeti ili kubo es a lugha yetu
- iii. \*Magazeti yanaan ikwa ili kuwa iza wanafunzi au wananchi yanayoendelea nchini

Wanafunzi waliacha sauti mbili /a/ na /z/ kwa neno **magazeti** na /s/ kwa neno **hawasomi**, katika neno **vizuri** na **kuboresha** sauti /z/, /b/ na /h/ ziliaachwa. Pia kwa neno **yanaandikwa** na **kuwajuza** sauti /d/ na /j/ zimedondoshwa na kuyafanya maneno hayo kutosheheni maana iliyotarajiwa. Kosa hili hutokea wakati wa kuandika kwa kasi kwa kuwa mawazo humjia mwanafunzi akilini kwa upesi. Kwa kuwa ni vigumu kuandika hivyo, kuna uwezekano wa kufanya makosa yanayotinga mawasiliano. Pia kosa la kudondoshwa kwa /h/ kwa neno

**kuboresha** lilisababishwa na athari ya lugha za kwanza za watafitiwa. Hii ni kwa sababu baadhi ya lugha za kibantu hawana sauti husika katika lugha zao.

#### 1.2.4 Lugha ya Kishairi

Lugha ya kishairi kwa kawaida ni tofauti na lugha inayotumiwa katika uandishi wa kawaida. Lugha hii huweza kufupishwa, kurefushwa, kutoholewa au kutofuata mpangilio wa maneno katika sentensi kwa minajili ya kupata idadi fulani ya mizani, au urari wa vina vya shairi husika. Lugha hii hukubalika tu katika utunzi wa mashairi pekee na mtunzi hawezi kulaumiwa na kukosolewa kuwa amevunja sheria za kisarufi. Wanafunzi wanapoitumia katika uandishi wa kawaida, maana iliyokusudiwa haimfikii msomaji kwa urahisi. Watu wengi hawaelewi hii lugha ya kishairi kwa kuwa ina upekee wake. Kauli zifuatazo zinadhihirisha matumizi ya lugha ya kishairi:

- i. *Ninaposoma magazeti selewe <sielewi>.*
- ii. *Palikuwa na storia kutoka kwa nyanya jana usiku <hadithi>.*
- iii. *Baba lakini sikumwona nilimtafuta mjini <Nilimtafuta baba mjini lakini sikumwona>.*

Mfano wa (i) wanafunzi walitumia lugha ya kishairi iitwayo inkisari (kufupishwa kwa baadhi ya maneno ili kupata idadi fulani ya mizani katika shairi. Neno ‘**selewe**’ ambalo lina mizani mitatu (3) limefupishwa kutoka kwa neno ‘**sielewi**’ ambalo lina mizani minne (4). Wanafunzi walipotumia mbinu hii walifanya kauli husika kutoeleweka kwa haraka. Neno **storia** katika (ii) lilitumiwa badala ya neno ‘**hadithi**’ ambalo lingeleta athari ile ile iliyokusudiwa na mwandishi. Neno hilo limetoholewa (lilishahiliwa moja kwa moja kutoka lugha ya Kiingereza) kutoka kwa neno ‘**story**’. Mpangilio wa maneno unaokubalika katika lugha ya Kiswahili katika (iii) haukuzingatiwa. Mwandishi aliyarundika maneno katika sentensi pasi kujua kama ujumbe unaeleweka au la na kusababisha makosa ya kisemantiki. Wanafunzi hufanya makosa husika kwa kutojua kuwa lugha ya kishairi ina uhuru wa kutozingatia kanuni za lugha sanifu na watunzi wa mashairi hawawezi kukosolewa au kulaumiwa. Baadhi ya walimu hufunza mashairi bila kuwatahadharisha wanafunzi athari ya kutumia lugha inayotumiwa katika uandishi wa mashairi katika uandishi wa insha au utungaji wa sentensi. Hivyo basi wanafunzi hutumia lugha hii ya kishairi bila kujua athari zake.

#### 1.2.5 Ufafanuzi Uliokithiri

Huu ni utumiaji wa maneno ya kuzungusha au maneno mengi yanayovuruga maana. Asemavyo Crowley (1982), kuna misukumo kadhaa ambayo inamfanya mwandishi kuhamisha maana ya maneno kutoka lugha asili hadi lugha ya pili. Hii hutokana na upanuzi wa maana. Iwapo mwandishi atabanwa na msamiati wa neno katika lugha ya pili, hupanua neno alilo nalo ili kukabiliana na hali inayomkanganya, kwa kufanya hivyo, ujumbe usiotarajiwa humfikia msomaji. Mfano:

- i. *Walevi wanaonywa na kutumia kwa wingi mapombe, sigara, marijuana, na kadhalika ili kuwa na kuishi katika hali yao isiyokuwa na magonjwa kwa maisha yao <Walevi wanaonywa dhidi ya utumiaji wa mihadarati ili kuwa na siha njema>.*
- ii. *Magazeti haya huwa na ilani ambazo humpa mwanafunzi ufaafu wa habari za kutenda vitu vya haina ya starehe, raha nyingi za dunia. <Magazeti huonya dhidi ya anasa za dunia.>*

Kutokana na kauli hizo, wanafunzi walikosa msamiati bora wa kujieleza. Katika (i) wanafunzi hajui neno ‘mihadarati’, badala yake anajieleza kwa maneno mengi kama vile ‘mapombe, sigara na marijuana. Pia alifanya kosa kwa kuongezea kiambishi ‘ma’ kwa neno pombe kuashiria wingi. Mdee (1988), anafafanua maana ya kiambishi asemapo:

“Ni mofimu inayowekwa kwenye mzizi wa neno na kukamilisha muundo wa neno. Kiambishi hubeba maana na kinaweza kuambishwa kabla na baada ya mzizi wa neno. Viambishi ni mofimu muhimu sana katika uundaji wa maneno mapya kutokana na mzizi wa neno moja.”

Kisarufi, kiambishi ‘ma’ katika neno ‘mapombe’ hakina maana yoyote, ila tu kulifanya neno husika kuwa na kasoro. Sharti ikumbukwe kuwa si maneno yote yanayoambishwa katika lugha ya Kiswahili, kwa mfano, nomino za pekee haziambishwi. Wanafunzi walijaribu kujieleza kwa lugha ya Kiswahili kutokana na mawazo yake ya lugha ya kwanza. Vilevile katika sehemu ya kauli ya (i) hapo juu, maneno mengi yalitumiwa (kuishi katika hali yao isiyokuwa na magonjwa katika maisha yao) badala ya kutumia msamiati unaofaa, ‘**siha njema**’. Brown (1994), ufafanuzi uliokithiri ni ishara ya mwanafunzi kuazima ruwaza kutoka kwa lugha ya kwanza na kutanua ruwaza katika lugha ya pili. Pia wanafunzi huwa na ujuzi wa kanuni za lugha fulani na anapojaribu kujieleza, hutumia kanuni za lugha hizo kwa kueleza hoja zake kwa lugha lengwa.

### 1.2.6 Mrundiko wa Maneno katika Sentensi

Kwa mujibu wa Tuki (1990), sentensi ni tungo iliyo na kiima kiarifu na yenye maana kamili. Sentensi ndiyo tungo ya juu kuliko kishazi na ambayo hujengwa na kishazi huru kimoja au kishazi huru kimoja na kishazi tegemezi kimoja. Sentensi huwa kipashio huru kimuundo na kikubwa zaidi kuliko vipashio vya kiisimu ambavyo hutumiwa kisarufi. Lugha zote za ulimwengu zina utaratibu maalumu katika upangaji wa maneno ili kuunda sentensi zenye maana. Kando na kuonyesha namna ambavyo maneno ya aina aina hufuatana katika sentensi kuunda sentensi, lazima uhusiano uliopo kati na baina ya viambajengo vya sentensi udhihirike. Lugha ya Kiswahili ikiwa mojawapo ya lugha za ulimwengu ina utaratibu wake ambao unastahili kuzingatiwa ili kuunda sentensi iliyokamilika kimaana. Kwa mfano, mojawapo ya kanuni za kiisimu ni kuwa, kivumishi hufuata nomino (huja baada ya nomino), kitenzi huja baada ya chagizo na kadhalika. Iwapo utaratibu huu hautazingatiwa katika utungaji wa sentensi, msomaji atatizika kung’amua maana iliyodhamiriwa. Kwa mfano:

i) *Sukari ilimwagika sakafuni yote na mtoto* <Mtoto alimwaga sukari yote sakafuni>.

ii) *Yule mtoto ameenda kumnunulia baba yake sokoni maziwa na maguu* <Mtoto yule ameenda sokoni kumnunulia baba yake maziwa kwa miguu>.

Katika mfano (i) hapo juu, mwanafunzi hakuzingatia utaratibu unaofuatwa katika utungaji wa sentensi katika lugha ya Kiswahili. Nomino tendewa imetangulia katika sentensi ikifuatwa na tendo. Vilevile chagizo inafuatwa na kivumishi halafu kiunganishi na hatimaye nomino tendi na kuifanya sentensi husika kuwa na makosa ya kisemantiki. Mfano wa (ii) ndio unaonyesha mrundiko wa maneno kiasi kwamba vitu vilivyounuliwa havieleweki. Maguu limetumiwa kama mojawapo wa vitu vilivyounuliwa. Mwanafunzi aliongeza kiambishi ‘ma’ kwa mguu ili kuleta dhana ya ‘miguu’ katika wingi na kupelekea sentensi husika kuwa na kasoro. Athari ya lugha za kwanza za watafitiwa ilipelekea kuwepo kwa kosa hili. Ellis (1994), akimnukuu corder (1970) anasema kuwa watu wanaojifunza lugha ya pili huwa tayari wanayo lugha ya kwanza.

Baadhi ya kanuni wanazozielewa katika lugha ya kwanza huzitumia katika usomaji na uandishi wa lugha ya pili.

### 1.2.7 Msimbo wa Sheng'

Hii ni lugha ambayo inayofahamika kama lugha ya vijana. Huwa ni lugha ambayo ni mseto wa lugha mbili au zaidi na ambayo kwa kawaida haizingatii kanuni za kisarufi. Msamiati wake hubadilikabadilika kwa vile sio mpana na wa kutegemewa. Uundaji wa maneno katika Sheng ni utaratibu changamani, unaohusisha mbinu tofauti na kufuata hatua kadhaa (Ogechi, 2002). Uundaji wake hutumia njia mbalimbali. Kuna matumizi ya ukopaji wa maneno kutoka lugha ya Kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za Kiafrika. Pia kuna kubuniwa kinasibu kwa maneno ya msimbo wa Sheng'. Shida huwa katika jamii-lugha yenye uwili-lugha na wingi-lugha kwa kuwa huathiri wanafunzi katika uundaji wa vitenzi, nomino na hata sentensi nzima.

Uundaji wa maneno katika msimbo wa Sheng hufuata sarufi ya lugha za Kibantu hususani Kiswahili. Kwa mfano '**alidhanywa**', kitenzi hiki kina 'a' ambayo ni kiima (nafsi), '-li-' ambacho ni kiambishi cha wakati (uliopita), '-dhany-' ni mzizi wa kitenzi. '-w-' ni myambuliko katika kauli ya kutendewa na '-a' ni kiishio. Hivyo basi, muundo wa Sheng unazingatia muundo wa Kiswahili sanifu ambao ni KI+KI. Watafitiwa walitumia msimbo wa Sheng kama inavyoonyeshwa katika kauli zifuatazo:

- i. *Baba alijenga hao nzuri kijijini* <nyumba>.
- ii. *Otish alitei pombe na kuwaka sana* na kupelekewa *hos* <Otieno, alikunywa, kulewa hospitali>.

Mifano iliyo hapo juu, imedhihirisha kuwa Sheng si lugha bali ni mchanganyiko wa msamiati unaotumiwa pamoja na sarufi ya Kiswahili. Hii ndiyo sababu Sheng huathiri lugha ya Kiswahili zaidi kuliko inavyoathiri Kiingereza. Katika (i) Sheng hufuata utaratibu wa sarufi ya Kiswahili. Neno 'hao' ambalo limefupishwa kutoka neno la Kiingereza, 'house' limechukua muundo wa sarufi ya Kiswahili, konsonanti + irabu + irabu (KII) ambalo linamaanisha 'nyumba'. Mfano katika (ii) majina halisi ya watu na mahali yameongezewa viambishi tamati **-sh** na **-s**. '**Otish**' na '**hos**' yamebadilishwa kwa kuongezewa kiambishi **-sh** na **-s** mtawalia. Kitenzi '**alitei**' ambacho kimezingatia muundo wa uundaji wa maneno katika Kiswahili, likiwa na maana ya 'kunywa' halieleweki moja kwa moja. Vilevile katika kitenzi '**kuwaka**' kiambishi 'ku-' kimeongezewa kwa kitenzi 'waka' na kuunda nomino ambayo ni kitenzi-jina iliyo na maana ya 'kulewa'. Maneno hayo yanapotumiwa katika sentensi huvuruga maana iliyodhamiriwa, kwa kuwa si wasomi wengi walio na umilisi wa msamiati wa Sheng. Pia, sentensi zinavurugika na maneno mengi huendelezwa visivyo kwa kutoheshimu ngeli za nomino. Sababu ya kushamiri na kuenea kwa msimbo wa Sheng ni kutokana na vijana kutaka kuzungumza mambo yao ya siri. Uvivu wa wanafunzi wa kutotaka kuandika maneno kikamilifu huchangia kuwepo kwa makosa husika. Msimbo huu huonekana kama unaotatiza ujifunzaji wa lugha nchini Kenya, ambazo ni Kiswahili na Kiingereza zinazotumika kuendesha masomo shuleni.

### 1.2.8 Kutumia Sauti Isiyofaa katika Neno

Matamshi ya maneno ya lugha yoyote ile ni mfumo wa sauti. Hali ya kutumia sauti moja mahali palistahili sauti nyingine tofauti, ilichangia kuwepo kwa kasoro katika baadhi ya maneno yaliyotumiwa na baadhi ya watafitiwa. Mawasiliano bora yatakuwepo iwapo sauti itatumika ipasavyo katika uandishi wa maneno. Wanafunzi hufanya kosa hili kwa kutumia sauti moja au



mbili mahali palipohitajika sauti nyingine tofauti. Matumizi hayo yalitokea kama inavyoonyeshwa hapa chini:

- i. *Baba alipokea mahali ya msichana wake* <mahari>.
- ii. *Yenye ana vutahi* <futahi>.
- iii. *Mwalimu alianguka jini alipokuwa akifundisha* <chini>.

Neno ‘**mahali**’ (i) lililo na maana ya sehemu ambapo kitu au mtu huweza kukaa limetumiwa badala ya neno ‘**mahari**’ ambalo linamaanisha mali au fedha inayotolewa na mwanamume kupewa mwanamke au wazazi wa mwanamke anayetaka kumwoa. Sauti ‘l’ na ‘r’ zilibadilishana nafasi kwa kuwa zote ni sauti za ufizi licha ya kuwa ‘l’ ni kitambaza na ‘r’ ni kimadende. Katika (ii) neno ‘**vutahi**’ limetumiwa badala ya neno ‘**futahi**’ ambalo lina maana ya bahati njema. Vivyo hivyo, neno ‘**jini**’ lililo na maana ya kiumbe asiyeonekana anayefikiriwa kuwa anadhuru watu badala ya neno ‘**chini**’ linalomaanisha kwenye sakafu au ardhi (TUKI, 1990). Baadhi ya sauti zilizobadilishwa huwa na sifa sawa (mahali pa kutamkiwa, na aina). Kwa mfano, sauti ‘v’ na ‘f’ zote ni vikwamizo na zinatamkiwa kwenye midomo na meno, hivyo basi, zinawakanganya wanafunzi wanapoandika matini yake. Hali hii hupelekea kuwepo kwa kasoro, kwa sababu maana iliyokusudiwa haitamfikia aliyedhamiriwa. Jamii-lugha nyingi huwa hazina baadhi ya sauti zilizobadilishwa hapo juu katika lugha zao za kwanza. Ellis (1994), anasema:

“Wakati watu wanapojifunza lugha ya pili huwa tayari wanayo lugha ya kwanza. Baadhi ya kanuni wanazozielewa katika lugha ya kwanza hutumiwa katika usemaji na uandishi wa lugha ya pili. Kuna mazoea ya kuzitumia kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili na hivyo makosa hutokea.”

Ni wazi kuwa sauti isiyofaa ilitumiwa katika maneno, mahali <mahari>, vutahi <futahi> na jini <chini>. Wanafunzi walikuwa na neno sahihi na alishindwa kubainisha maendelezi mwafaka katika maneno husika. Maana ya maneno yaliyotumiwa katika nafasi za maneno yaliyostahili yalipelekea kuwepo kwa makosa ya kisemantiki. Kosa hili hutokana na matamshi ya watafitiwa ambayo yalihamishwa kutoka lugha zao za kwanza katika uandishi wa insha zao. Kuandika kwa kasi pia kunawafanya kutenda kosa hili.

## 2.0 Mapendekezo

Washikadau anuwai wanahitajika ili kuboresha mawasiliano andishi ya Kiswahili. Rai ya makala haya ni kwamba, makosa yashughulikiwe kwa njia ya kipekee kwa kuwa yanatatiza uelewekaji wa ujumbe. Walimu wawapatie wanafunzi kazi nyingi za kuandika shuleni na nyumbani ili kuimarisha mawasiliano andishi. Walimu wasahihishe makosa yanayotatiza uelewekaji wa ujumbe. Watumie mbinu anuwai katika kufunza kuandika kama vile kuwapa wanafunzi kazi ya makundi, nafasi ya uigizaji na kujadiliana. Watumie mbinu zinazowapa wanafunzi motisha katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Ni wajibu wa walimu kuwaelekeza wanafunzi kwenye mchakato wa kuandika matini.

Wanafunzi waache uvivu. Wasome vitabu vingi vya lugha ya Kiswahili ili kuwa na umilisi wa matumizi ya Kiswahili sanifu. Kwa kufanya hivyo, watafahamu miundo mbalimbali ya sentensi za Kiswahili, matumizi ya aina mbalimbali za maneno na nafasi inayostahili kuachwa kati ya neno moja na lingine. Waandike matini mbalimbali kadri wanavyoweza ili kuimarika katika uandishi wao. Wapatie kazi zao wamalizapo kuziandika ili kurekebisha makosa yaliyojitokeza walipokuwa wakiandika kwa haraka. Watumie kamusi ya Kiswahili sanifu ili kufahamu maana

ya msamiati ambao unawatatiza. Watumie lugha sanifu ya Kiswahili katika mandhari na miktadha halisi ili waweze kukuza ufasaha na umilisi wao katika mazungumzo na uandishi.

Taasisi ya ukuzaji mitaala nchini Kenya, itilie mkazo vipengele vinavyowatatiza wanafunzi katika uwasilishaji wa ujumbe katika mawasiliano andishi ya Kiswahili. Wachunguze vitabu vinavyotumiwa katika suala nzima la ufunzaji wa Kiswahili katika shule za msingi na za upili, nchini Kenya. Watathmini kiwango cha msamiati ambao umetumiwa katika uandishi wa lugha ya Kiswahili ili kuboresha mawasiliano andishi ya Kiswahili. Watunzi wa mashairi wahimizwe kutumia Kiswahili sanifu katika utunzi wao wa mashairi.

### 3.0 Hitimisho

Katika makala haya tumejadili makosa mbalimbali ya kisemantiki ya wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya. Makosa yaliyojadiliwa ni pamoja na: Matumizi ya msamiati usiofaa; kuunganishwa kwa maneno visivyo; kuacha neno katika sentensi; matumizi ya lugha ya ushairi; ufafanuzi uliokithiri; mrundiko wa maneno katika sentensi; matumizi ya msimbo wa Sheng na kutumia sauti isiyofaa katika neno. Hata hivyo, tumedondoa mifano anuwai kwa kila kosa kama ilivyojitokeza katika data yetu (matini za wanafunzi wa shule za upili hususani kidato cha tatu, kaunti ya Kakamega). Pia, baadhi ya vyanzo vya makosa husika vilivyobainishwa ni pamoja na: athari ya lugha za kwanza za watafitiwa, athari ya msimbo wa Sheng, ukiukaji wa sheria za lugha lengwa na athari ya lugha ya kishairi. Hatimaye, makala haya yamependekeza hatua mbalimbali zinazostahili kutiliwa maanani ili kupunguza utokeaji wa makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya wanafunzi wa shule za upili.

### Marejeleo

Asiba, A.(1995, August 30). *Can Sheng Stand the Test of Time*. Sunday Nation Nairobi, p9

Brown, H.D. (1987). *Principles of Language Learning AND Teaching*. Retrieved May 10, 2014 from <http://www.google.com>.

Corder, S. P. (1967). *The Significance of learners Errors*. Reprinted in J. C., Richards (Mh) (1974, 1984) *Error Analysis: Perspective on second Language Acquisition*. London: Longman. Reprinted January 12, 2014 From <http://absamra03.tripod.com/.../languageacgerranalysis.htm>.

Crowley, T. (1982). *An Introduction to Historical Linguistic*. Oxford: O.U.P.

Ellis, R. (1994). *The Study of Second Language Acquisition*. Oxford: Oxford University Press.

Cruse, D. A. (1986). *Lexical Semantic*. Cambridge: Cambridge University Press.

Fauconnier, G. (1997). *Mapping in Thought and Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Griffiths, P. (2006). *An Introduction of English Semantic and Pragmatic*. Edniburgh: Edniburgh University Press.

Habermas, J. (1979). *What is Universal Pragmatics?* Trans. Thomas McCathy, *Communication and Evolution of Society*. BOSTON: Beacon, 1-68.

- Jackendoff, R. (1987). *Semantic Structure*. Cambridge MA: MIT Press.
- James, C. (1998). *Errors in Language Learning and Use, Exploring Error Analysis*. Harlow: Longman.
- Katz, J. (1986). *Common Sense in Semantic. New Directions in Semantic*. New York: Academic Press.
- K.I.E (200). *Guidelines of Early Childhood Development in Kenya*. Nairobi: National Centre for Early Childhood Education. Retrieved from [www.moh.gov.rw/](http://www.moh.gov.rw/)
- Lakoff, G. (1988). *Cognitive Semantic, Meaning and Mental Representation*. Bloomington Indian: University Press.
- Mdee, J. S. (1986). *Kiswahili Muundo na Matumizi yake*. Dar es Salaam: Dar es Salaam International Publishers Ltd.
- Mgullu, R.S. (1999). *Mtaala wa Isimu: fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longman Publishers.
- Newmeyer, F. J. (1993). *Grammatical Theory. Its Limits and Its Possibilities*. Chicago University: Chicago Press.
- Obeidat, H. (1986). Syntactic and Semantic Errors. In James (1998). *Errors in language Learning and Use Exploring Error Analysis*. Harlow: Longman.
- Obuchi, S. M. na Mukhwana, A. (2010). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele*. Nairobi: A~Frame Publishers.
- Ogechi, N. O. (2002). *Trilingual Codeswitching in Kenya: Evidence from Ekegusii, Kiswahili, English and Sheng*. Hamburg: University of Hamburg.
- Ponter, P. (2005). *Whats meaning? Foundation of Formal Semantic*. Malden, MA: Blackwell
- TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Tyler, A. na Evans, V. (2003). *The Semantic of English Preposition; Spatial Scenes Embodied Meaning and Cognition*. Cambridge: University Press.
- Wyrick, J. (1979). *Steps to Writing Well: A concise Guide to Composition*. New York: Holt, Rinehart & Winston.
- Zimmermann, R. (1986). Semantic and Lexical Errors Analysis. *English Amerikasche Studien*, 2(86) 294-305.